JINA: .......................................NAMBARI YA MTAHINIWA: ..............

SHULE ....................................... MKONDO: .......................................

SAHIHI YA MTAHINIWA.........................TAREHE ................................

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
Juni
Muda: Saa 2 ½

MUUNGANO WA BUNYORE-MARANDA (BUMA II)
MTIHANI TANGULIZI MWIGO (KIMWIGO)

MAAGIZO

(a) Andika jina lako, nambari yako ya mtihani, jina la shule yako Na mkondo wa darasa lako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali yote
(d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali
(e) Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki
(g) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopiga chapa
(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawaswa na kuwa maswali yote yamo.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | | |

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Tangu opresheni ya Usalama kuanza kutekelezwa na maafisa wa usalama katika mtaa wa Eastleigh, kumekuwa na propaganda kuwa inalenga watu wa jamii na dini Fulani.

Harakati hizi za kuwasaka magaidi sharti ziendelee na zichangiwe na kila raia ili zizae matunda atunayoazimia kupata; kuwanasa wote wanaohusika.

Wakenya tumeishi kwa miaka mingi bila kubaguana katika misingi ya dini na ukabila. Iweje tuanze sasa miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru? Nidposa tunawasihi Wakenya wote wenye nia njema kukumbuka kwamba hatuna njia ya mkato katika suala hili la ugaidi. Sharti tupambane nao. Hawa ni watu; ni ndugu zetu, rafiki zetu na watoto wetu.

Hakuna mzazi atakayejitokeza hadharani na kukiri kuwa mtoto wake ni gaidi! Hata kama atajua wazi mwanawe ni gaidi na amelipua Wakenya na ataendelea kufanya hivyo akizidi kupewa nafasi. Atanyamaza na kumtetea kwa hali na mali.

Madhara ya mashambulizi hayo ya kigaidi tayari yameanza kuonekana ambapo wamiliki wa mahoteli ya kifahari wanalalama kuwa idadi ya wageni imepungua maradufu. Hali kama hii ni hatari kwa uchumi wa nchi.

Sis tukiwa Wakenya wapenda amani hatuna budi kuungana mkono katika opersheni hiyo na kushirikiana na maafisa wa usalama kwa kutoa habari muhimu kuhusu washukiwa wa ugaidi. Hakuna operesheni dhidi ya wahalifu ambayo inaweza kuendeshwa bila jamii ambapo wamejificha kuathiriwa. Heri nusu shari kuliko shari kamili; magaidi wana madhara makuba kuliko operesheni ya usalama.

Sisi Wakenya kwa sasa tuko katika hali hii tatnishi ya kushindwa kuamua; tupambane na magaidi tuumize na Wakenya wachache wasio na hatia ama tuache tu magaidi wakae kwa sababu tunaogopa kuwasumubua hao wachache.

Kadhalika, badala ya kuangazia maeneo yenye visa vingi vya mashambulizi ya ugaidi operesheni ya usalama inafaa kuelekezwa pia katika maeneo mengineyo ambayo yamekuwa yakikumbwa n avisa vya utovu wa usalama mara kwa mara.

Vikosi vya usalama vinafaa kuhakisha kuwa magenge ya aina hii hayasazwi katika operesheni hiyo. Aidha, serikali inapaswa kutoa makataa kwa kila Mkenya ambaye anamiliki bunduki ikinyume cha sheria kusalimisha silaha hizo mara moja katika vituo vya polisi, la sivyo wachukuliwe hatua kali za kisheria.

Wakenya wote wafaa kuonyesha ushirikiano kwa kuwa makini zaidi. Wajiepushe na maeneo hatari ambayo yaweza kuwa makazi ya magaidi ama ya washukiwa wa ugaidi. Aliye kando haangukiwi na mti ama mshausahau huo maarufu.

(a) (i) Eleza uongo unaosambazwa kuhusu operesheni ya usalama mtaani Eastleigh. (alama 1)

(ii) Operesheni hii ina lengo lipi? (alama 1)

(b) Eeleza jinsi Wakenya wamekuwa wakiishi tangu uhuru. (alama 1)

(c) (i) Magaidi wana uhusiano upi nasi kwa mujibu wa kifungu? (alama 1)

(ii) Eleza namna wazazi wanavyochangia kuwepo kwa ugaidi nchini. (alama 2)

(d) Fafanua athari mbili zinazokumba nchi kutokana na ugaidi. (alama 2)

..............................................................................................................

(e) Wakenya wamepewa changamoto ipi ili kusaidia kaitka uangamiza ugaidi? (alama 2)

..............................................................................................................

(f) "Wakenya wako kwenye njia panda." Tetea kauli hii ukirejelea kufungu. (alama 2)

..............................................................................................................

..............................................................................................................

(g) Serikali inapaswa kuchukua hatua ipi dhidi ya wamiliki haramu wa bunduki? (alama 2)

(h) Eleza maana ya methali hii kulingana na taarifa. (alama 1)
Aliye kando haangukiwi na mti.

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Sma kifungu kifauatacho kisha ujibu maswali.

Mifuko ni muhimu sana katika maisha ya binadamu ya kila siku. Baadhi ya mifuko huundwa kwa namna ambayo inadumu na inaweza kutumiwa mara kadha wa kadha. Hii huweza kuhifadhiwa na kutumiwa kwa kipindi kirefu. Asilimia kubwa ya mifuko ya aina hii hutengenezwa kutokana na nguo au ngozi. Hata hivyo, ipo mifuko mingine ambayo si ya uashi, haidumu. Hii ni mifuko myepesi, rahisi kubebeka na inayopatikana kwa wingi sana. Hii ni mifuko ya plastiki.

Mifuko ya plastiki hupatikana katika maeneo mengi sana. Mifuko hii sio ghali inapolinganishwa na ile ya nguo au ya ngozi. Hii ni ya gharama ya chni na hupendwa kutokana na wepesi wake. Hata hivyo, mifuko hii inaweza kuwa chanzo cha matatizo mengi. Matatizo haya hutokana na linalopasa kufanywa kuhusu mifuko hii baada ya kutumiwa kwake. Mifuko ya nguo ambayo inatupwa kwenye jalala huishia kuoza na kuwa sehemu ya uchafu wa jalala hilo. Kwa upande wake, mifuko huo. Hata inapofukiwa arthini haiwezi kuoza hata kama kufukiwa huko ni kwa miaka mingi. Aidha hata pale inapochomwa, haiwezi kuteketea hadi kuwa jivu kama ilivyomifuko ya karatasi.

Upo umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa sera madhaubuti za kupambana na tatizo la mifuko hii. lazima zitungwe sheria ambazo zinakabiliana na-uchafuzi wa mazingira kwa njia hii. kwa njia hii hatari zianzowakabili watu na wanyama zitapunguzwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hakika njia mojawapo ambayo ingeweza kutumiwa ni kuharamisha matumizi ya mifuko hii katika upakiaji. Sheria zinaweza kupitishwa ambazo zinahimiza matumizi ya mifuko mbadala kama ile ya karatasi kubebea vitu vidogo Fauka ya hayo, pana haja ya kuwazia kuwepo kwa njia nzuri kuteketezea mifuko hiyo. Inawezekana kuhimiza watumiaji kuirejesha mifuko hiyo mahali Fulani kwa ajili ya uteketezaji huo. Hata hivyo, hali hii huenda ikawa ngumu kwa kuwa inahitaji nidhamu ya hali ya juu sana kwa upand ewa watumiaji.

(a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za mwanzo kwa maneno 105 – 110.(alama 10, 1 utiririko)
Matayarisho

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

Nakala safi

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Eleza mawazo makuu yanayojitokeza kaitka aya ya mwisho (maneno 50 – 55) (alama 5, 1 utiririko)

Matayarisho

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

Nakala safi

..............................................................................................................................

.....................................................................................................................

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) (i) Kipashio kikubwa zaidi katika ujenzi wa lugha kinaitwaje? (alama 1)

.....................................................................................................................

(b) Andika sauti mbili ambazo ni vikwamizo vya mdomo wa meno. (alama 2)

.....................................................................................................................

(c) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika usemi wa taarifa. (alama 2)

"Nitawafundisha usemi wa taarifa kesho," mwalimu alituambia.

(d) Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha nomino. (alama 2)

.....................................................................................................................

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi. (alama 4)

Wanafunzi wenye bidii masomoni hufuzu mtihani.

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

(f) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)

Baba alipashwa habari kwa rununu.

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

(g) Tambua muundo wa virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo: (alama 2)

(i) Mikakati iliyobuniwa na serikali itaimarisha usalama nchini.

.....................................................................................................................

(ii) Mara nyingine msimu wa masika umewadia.

(h) Andika upya sentensi zifuatazo kwa kuzingatia kauli zilizomo mabanoni. (alama 2)

(i) Watoto wenyewe wamekunywa maziwa yao yote. (tendwa)

(ii) Pombe haramu inawafisha Wakenya wengi. (Badilisha kitenzi kiwe nomino)

(i) Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha matumizi yafuatayo ya ndivyo. (alama 2)

(a) Jinsi

(b) Kirejeshi cha kuthibitisha.

(j) Eleza maana tatu zinazoibuliwa na vitate vilivyotumika katika sentensi hii. (alama 3)

Bosi wetu ana pozi nyingi lakini ni bozi sana.

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa.

Uso wa kijana Yule ulichujuka alipoanguka. (alama 2)

..........................................................................................................................

(l) Eleza matumizi mawili ya viakifishi vifuatavyo: (alama 4)

(i) Herufi nziot (H) / zilizokolewa.

..........................................................................................................................

(ii) Mstari

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

..........................................................................................................................

Bainisha mofimu za: (alama 3)

Nitakujia

..........................................................................................................

(m) Unganisha sentensi hizi kwa kutumia kirejeshi cha kati mwafaka. (alama 1)

Gari limeibwa. Gari ni langu.

(n) Ainisha vihusishi katika sentensi hizi: (alama 2)

(i) Mwanafunzi huyu ni mwerevy sana kuliko wenzake wote.

..........................................................................................................

(ii) Tangu apate mamlaka amepuuzxa wadogo wake.

..........................................................................................................

(o) Unda kitenzi kutokana na neon "Zawadi" (alama 1)

..........................................................................................................

(p) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Ingawa amefunga bao hajacheza kwa muda.

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

USAJILI WA WATAHINIWA

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewaagiza walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari wabandike hadharani orodha ya watahiniwa wote waliosajiliwa ili kuwawezesha wazazi na walimu kuthibitisha maelezo yote ya usajili.

Kwenye taarifa aliyoitoa kwa vyombo vya habari, Waziri Prof. Kaimenyi alitoa wito kwa wazazi na wanafunzi watakaofanya mitihani ya kitaifa mwaka huu wa 2014 wahakikishe kuwa watahiniwa wamesajiliwa vilivyo. Aliwataka wathibitishe usajili wao katika tarakilishi na kutia saini nakala hizo kama inavyohitajika.

(a) Tambua sajili ya makala haya. (alama 2)

(b) Eleza sifa nane za kimsingi za sajili hii. (alama 8)

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................

..........................................................................................................